

Mpangilio

Mshikano wa Benki ya Dunia unajumuisha mashirika matano yanye uhusiano wa karibu. Mashirika yote haya yanamilikiwa na nchi wanachama zenye uwezo kamili wa uamuzi. Kama ilivyoelezwa hapa chini, kila shirika lina kazi muhimu katika juhudi za kupigana na umasikini na kuimarisha hadhi ya maisha ya watu wanaoishi katika nchi zinazoendelea. Neno "World Bank Group" [Mshikano wa Benki ya Dunia] hujumuisha mashirika yote hayo matano. Neno "World Bank" [Benki ya Dunia] linajumuisha mashirika mawili tu kati ya haya matano, IBRD na IDA.

The International Bank for Reconstruction and Development [Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo]

Ilibuniwa 1945 Wanachama 184

Jumla ya Mikopo: bilioni \$360

Mikopo kwa Mwaka wa Fedha 2002: bilioni \$11.5 kwa miradi 96 mipya katika nchi 40

IBRD ina nia ya kupunguza umasikini katika nchi zenye pato la kati, na pia zenye kustahili kuomba mikopo kwa kusaidia maendeleo ya kudumu kupitia mikopo, hakikisho, na kwa njia za kutokopesha-zikiwema huduma za ukaguzi na kupeana wasia. IBRD haizidishi faida yake balli imeweza kuwa na pato kamili la sawa tangu 1948. Faida zake hufadhili shughuli mbalimbali za maendeleo na uhakikisha kuweko kwa uwezo wa kifedha ambao huwezesha kukopesha kwa wastani katika masoko ya fedha, pamoja na kuweko kwa masharti mazuri kwa wateja wanao kopoeshwa. Ikiwa inamilikiwa na nchi wanachama, IBRD hupatanisha uwezo wa kupiga kura na mchango wa pesa za wanachama kulingana na uwezo wa kiuchumi wa nchi.

The International Development Association [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo]

Ilibuniwa 1960 Wanachama 162

Jumla ya Mikopo: bilioni \$135

Mikopo kwa Mwaka wa Fedha 2002: bilioni \$8.18 kwa miradi 133 mipya katika nchi 62

Michango kwa IDA inaiwezesha Benki ya Dunia kupeana bilioni \$6 hadi 7 kwa mwaka kwa karadha bila ya mikopo kwa nchi 78 zilizo masikini zaidi ambako kunaishi watu bilioni 2.4. Msaada huu ni wa muhimu sana kwa sababu nchi hizi hazina uwezo wa dhati wa kukopesha kwa kupitia mipango ya soko. Katika nyingi ya nchi hizi mapato ya kawaida hayazidi \$500 kwa mwaka kwa kila mtu, na watu wengi zaidi wanalazimika kuishi kwa pato la haat chini zaidi. IDA inasaidia kuhakikisha kuweko kwa huduma muhimu (kama elimu, afya, maji masafi na usafi wa jamii) na inasaidia mageuzi na uwekezaji wenye lengo la kukuza mazao na kuleta ajira.

The International Finance Corporation [Muungano wa Kimataifa wa Fedha]

Ilibuniwa 1956 Wanachama 175

Kujitolea kwa mikopo: bilioni \$21.6 (pamoja na bilioni \$6.5 za mikopo [syndicated])

Kujitolea kwa mwaka wa fedha 2002: bilioni \$3. (pamoja na syndications, bilioni \$2.7 kwa akiba yake binafsi) kwa kampuni 204 kwa nchi 75.

Madaraka ya IFC ni kuelekeza maendeleo ya kiuchumi kupitia sekta ya kibinafsi. Pamoja na washiriki wa kibiashara, inafanya uwekezaji katika biashara za kustawi za kibinafsi katika nchi zinazoendelea na inapeana pia mikopo ya mda mrefu, hakikisho, na usimamizi wa hasara na huduma za wasia kwa wateja wake. IFC inawezeza katika miradi ya sehemu na sekta zenye uwekezaji duni wa kibinafsi na pia hutafuta namna za kupatikana nafasi katika masoko yanayodhaniwa na wawekezaji wa kibiashara kuwa yanaweza kuleta hasara pasipo kuwa na ushirikiano wa IFC.

The Multilateral Investment Guarantee Agency [Shirika la Uthibiti wa Uwekezaji]

Ilibuniwa 1988 Wanachama 157

Jumla ya fedha za uhakikisho zilizopenwa: bilioni \$10.34

Mwaka wa fedha 2002 guarantees zilizopenwa: bilioni \$1.36 (vikiwemo viinua uchumi vya milioni \$136 kupitia Cooperative Underwriting Program [Mpango wa Uwandikishaji wa Mashirika].)

MIGA inasaidia kutillia moyo uwekezaji wa kigeni katika nchi zinazoendelea kwa kuwahakikishia wawekezaji wa kigeni usalama dhidi ya hasara zinaotokea kwa sababu ya athari zisizokuwa za kibiashara, kwa mfano, matumizi mabaya ya fedha, kutoweza kubadilika kwa pesa za kigeni, vikwazo vya utumaji wa pesa, vita na misukosuko ya kijamii. MIGA pia hupeana usaidizi wa kiufundi ili kusaidia mataifa yasambaze ujumbe wa nafasi za uwekezaji. Shirika hili pia husaidi kwa utatuzi wa mizozo ya uwekezaji linapo ombwa kufanya hivyo.

[ICSID The International Centre for Settlement of Investment Disputes](#) [Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Mizozo ya Uwekezaji]

Ilibuniwa 1966 Wanachama 134

Jumla ya kesi zilizoandikishwa: 103

Mwaka wa Fedhal 2002 kesi zilizoandikishwa: 16

ICSID inasaidia kutillia moyo uwekezaji wa kigeni kwa kuandaa mbinu za kimataifa za Utatuzi wa Mizozo ya Uwekezaji. Kwa namna hii inasaidia kuwoko kwa hali ya imani kati ya mataifa na wawekezaji wa kigeni. Maelewano mengi ya kimataifa kuhusu uwekezaji hutumia mbinu za utatuzi za ICSID. ICSID pia ina upana na kazi za uchapishaji katika nyanja za sheria ya utatuzi na sheria ya uwekezaji wa kimataifa.